OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI

SHULE YA SEKONDARI
SERENGETI
S.L.P 46
MUGUMU-SERENGETI

NAMBA ZA SIMU
0684-420316
0624-192717

MZAZI/MLEZI WA ……..
S.L.P ……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SERENGETI KIDATO CHA TANO, 2018/2019

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii ya sekondari Serengeti mnamo Julai 2018 katika tahasusi ya HGL/HKL*(futa isiyohusika)* Shule ya sekondari Serengeti ipo umbali wa kilometa 04 kusini mwa mji mdogo wa MUGUMU, ambao ndio makao makuu ya wilaya ya Serengeti. Usafiri kutoka mjini kuja shuleni unapatikana kwa pikipiki, nauli ni Tsh 1500/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 02.07.2018. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia siku ya ijumaa na mwisho wa kuripoti.

2.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 Sare Ya Shule

a)Sketi mbili (02) za rangi ya **kijanijeshi/kombati** kitambaa kizito namba moja cha suti zenye marinda ya kawaida kumi na mawili (12)zinazovuka magoti
b) Shati mbili (02) nyeupe zenye mikono mirefu.ziwena mfuko mmoja tu.
c) Tai mbili (02) za rangi ya pundamilia(mistali inayokatisha) mieupe na kijani.
d) Fulana/ T’ shirt mbili (02) za rangi ya blue nyeusi (dark blue) zenye kola.
e) Viatu vya ngozivyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
f)Soksi jozi mbili nyeupe nzito zisizo na alama/mistali yoyote.
g) Sweta mbili (02) rangi ya **kijanijeshi/kombati** kwa ajili ya baridi
h)Nguo za kushindia (shamba dress) gauni (02) mbili kitambaa cha kunguru chenye miraba ya rangi nyeupe na blue bahari (light blue).mshono aina ya solo isiyo na marinda yeyote.
i) Track suit moja (01) ya rangi ya dark blue (blue nyeusi)

j) Rangi ya hijab (kijuba) nyeupe isiyokuwa na urembo wowote.(**kwa waislamu tu**).
k) Raba nyeupe za michezo jozi moja. Pamoja na bukta moja au track suit ya rangi ya blue kwa ajili ya michezo.
.
Kumbuka: Kama utapata utata/shida katika kutambua rangi za sare ya shule zinsi tulivyokuelekeza hapo juu, tafadhali njoo na fedha utapata maelekezo zaidi jinsi ya kuzipata huku **Mugumu**.

2.2 Ada Na Michango Ya Shule
a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/=. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa yote kwa mara moja. Fedha hizo pamoja na michango mingine ya shule zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na 30201200053, Jina la Akaunti ni SERENGETI SECONDARY SCHOOL RECURENT A/C NMB MUGUMU. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

B) Michango Inayotakiwa Kulipwa Na Kila Mzazi Ni;
i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na matroni
v) Shilingi 2,000/= nembo ya shule
vi) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza, **shule haitahusika kugharimia matibabu** ya mwanafunzi zaidi ya huduma ya kwanza, hivyo tunashauri kila mwanafunzi ajiunge kwenye mifuko ya bima ya afya.(NHIF au CHF),
vii) Shilingi 10,000/=kwa ajili ya kukodisha godoro kwa muhula, magodoro yanapatikana shuleni.
viii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya mtihani wa kujipima mock
ix) Shilingi 5000/= kwa ajili ya tahadhali (fedha hii haitarejeshwa)
Kumbuka. Fedha zote hizi zilipwe kwenye Account ya shule tuliyoweka hapo juu. Na aje na pay in slip ya benki na aikabidhi kwa muhasibu siku ya kuripoti.

C) Mahitaji Muhimu Ambayo Mwanafunzi Anapaswa Kuleta/Kuja Nayo Shuleni Ni;
i) Ream ya karatasi 1 moja (A4) aina ya Double A
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika anayokuja kusoma mwanafunzi
iii) Godoro Futi mbili na nusu (75cm) kwa wale ambao wataamua kuja na magodoro yao.
iv) Mashuka pair 2, pair Moja rangi ya pinki na nyingine rangi ya blue. Blanket 1, foronya 1 yenye rangi inayofanana na mashuka, chandarua kimoja 1 chenyerangi ya blue kinachoendana na godoro.
v) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
vi) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
vii) dumu la lita tano (05) kwa ajili ya kuhifadhia maji yake ya kunywa.
viii) Ndala au viatu vya wazi kwa ajili ya kuogea na kushindia.
ix)) Taulo moja(01) kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi.
x) Sanduku la kuhifadhia vifaa vyake. (**Tunashauri liwe la chuma/batigumu kwa ajili ya usalama zaidi**
xi) Jembe 01 lenye mpini wake.
x) Reki 01 yenye mpini wa chuma
xi) Mfagio laini wa ndani mmoja (01)
xi) Mahitaji muhimu mfano pedi, dawa ya meno, miswaki n.k yasisahaulike.
xii) Madaftari makubwa (Counter books) saba au zaidi.
xiii) Scientific calculator kwa wanafunzi wa HGL**. (sio lazima)**

xiv) Kalamu za kutosha

MUHIMU: **NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KUVALIWA HAPA SHULENI, HIVYO ASIJE NAZO KABISA**.

3.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi) Kusuka nywele au kuwa na nywele ndefu shuleni. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.
vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii) Uvutajiwasigara
ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuolewa au kuoa
x) Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiv) Kudharau Bendera ya Taifa
xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n,k
xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4.0 USAJILI

Mwanafunzi atasajiliwa katika ofisi ya makamu mkuu wa shule. Hivyo atatakiwa kukabidhi fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itakuwa imejazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali**.(fomu hii imeambatanishwa nyuma**)

Vilevile atakabidhi maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai. Pamoja na hivyo atakabidhi Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni,kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Na mwisho atakabidhi picha NNE (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

(**Picha hizi ziwe za watu ambao majina yao yameandikwa katika fomu maalumu tuliyoambatanisha nyuma**)

Tafadhali soma kwamakinimaelekezo haya na uyatekelezekikamilifu.

“KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SERENGETI”

JUVENALIS J.CHACHA
KAIMU MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI SERENGETI
FOMU YA UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

SEHEMU A: TAARIFA YA MWANAFUNZI

Jina la Mwanafunzi ----------kidato cha ----------mwaka ------
Shule ya sekondari niliyosoma“O level” ----------ilipo wilaya ya----------
nimechaguliwa kusoma tahasusi ya HGL/HKL (futaisiyohusika).

SEHEMU B : TAMKO LA MWANAFUNZI

Mimi ----------nakiri kuwa nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule
Kwa makini. Na naahidi kuwa;
“Nitazifuata sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoelekeza Aidha ninaamini kuwa sheria na taratibu zote za shule zipo kwa lengo la kunisaidia kinidhamu na kitaaluma”.
Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu. Nakili haya mbele ya mzazi/mlezi wangu.
Jina la mwanafunzi ----------sahihi----------
Jina la mzazi/mlezi ----------sahihi----------

SEHEMU C: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI NA NDUGU

i) Jina la baba ---------- anaishi----------wilaya----------
Kazi yake ni ----------anuani yake ni ---------- na.yasimu----------

ii) Jina la mama ---------- anaishi ----------wilaya----------
Kazi yake ----------anuani yake ni ----------na ya simu----------

iii) Jina la ndugu ----------anaishi----------wilaya ya ----------
Kazi yake ----------anuani yake ni ---------- nay a simu----------

iv) Jina la ndugu ----------anaishi ----------wilaya ya ----------
Kazi yake ----------anuani yake ni ----------na ya simu----------

TAMKO LA MZAZI/MLEZI

Mimi ---------- Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ----------
--Ninaahidi kulipa ada na michango mingine yote kama ilivyoelekezwa kwenye fomu yake ya kujiunga na shule ya sekondari Serengeti. Aidha nakiri kukubalianana sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. Naahidi kushirikiana na uongozi wa shule ya sekondari Serengeti katika kumlea mwanangu katika misingi inayofaa.

Sahihi ya mzazi/mlezi ----------

Jina la mzazi/mlezi ----------

Namba ya simu ----------

SERENGETI SECONDARY SCHOOL

SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO THE MEDICAL OFFICER

Name of student ----------
Form ---------- Term ---------- Year ----------

Dear Doctor

Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )
4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6. Tuberculosis ( )

A: (I) PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)

NO	DISEASE	YES/NO	NO	DISEASE	YES/NO
1	Tuberculosis		10	Epilepsy	
2	Pneumonia		11	Ear, Nose and threat	
3	Asthma		12	Skin disorder disease	
4	Heart trouble		13	Anemia	
5	Recurrent indigestion		14	Operations	
6	Jaundice		15	Serious Accident	
7	Dysentery		16	Malaria	
8	Kidney and urinary trouble		17	Stomach trouble	
9	Nervous breakdown		18	Eye disorder	

(II) VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISOTRY

DISEASE	1ST DATE	2ND DATE	3RD DATE
Small pox			
Whooping cough			
Measles			
Yellow fever			
Cholera			

Official

B: MEDICAL EXAMINATION REPORT

(a) Weight

(b) Heat Beat

(c) Vision etc

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.

DOCTOR'S NAME & SIGNATURE ----------

DATE ----------